

na kuzua mwenyeji wa haki na potofu wa soko.

wa shakabaa ghafla hema, Asangye Bangu. Mkulima kutoka wilayani

korosho walizopewa msimu huu hazikidhi mahitaji ya waku-

wakati. "Ndiyo maana hata Mkuru-

kuongeza uzalishaji wa korosho.

HABARI LEO UK 17.

Mil 73.5/- kuboresha machinjio, minada

Na John Nditi, Kilosa

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro imetenga Sh milioni 73.5 kwa ajili ya uboreshaji mkubwa wa miundombinu katika minada ya mifugo kuongeza mapato yato-kanayo na mazao ya mifugo.

Minada hiyo ni ya Rudewa, Mbwa pamoja na machinjio ya Masugu na Kimamba.

Ofisa Mifugo wa halmashauri hiyo, Dk Yuda Mgeni alisema hayo

hivi karibuni kwenye mkutano wa wadau wa kilimo, mifugo na uvuvi kutoka ndani na nje ya wilaya, chini ya mwenyekiti ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Majid Mwanga.

Dk Mgeni alisema kiasi hicho kimetengwa kutoka kwenye mapato ya ndani katika bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema licha ya uboreshaji wa miundombinu hiyo, halmashauri pia imetenga Sh milioni 15.1 kwa ajili ya kuboresha huduma za ugani katika sekta ya mifugo na uvuvi.

Alisema ili kukuza kipato cha wafugaji, idara imewezesha kupan-

dikiza vifaranga vya samaki 20,000 aina ya sato katika mabwawa ya asili na kuboresha uzalishaji wa samaki. Imewezesha pia vikundi saba vya ufugaji samaki kwa kuvipatia vifaranga 6,000 vya samaki.

Alisema kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi pamoja na wadau ikiwamo wafugaji, wamechangia shughuli za uboreshaji wa miundombinu ya afya ya mifugo, hususani malambo na majosho.

Alisema halmashauri kwa kushirikiana na Chama cha Wafugaji, Wilaya ya Kilosa itaendelea

kutoa elimu kwa wafugaji juu ya umuhimu wa usajili mifugo kupitia mikutano na vikao vya wafugaji.

Katika hatua nyingine, halmashauri hiyo imeandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi katika vijiji 36 na kutenga maeneo ya malisho ekari 225,149 kwa ajili ya ufugaji wa asili.

Mgeni alisema eneo hilo la malisho lina uwezo wa kuhifadhi mifugo 112,575 kwa kipindi cha mwaka mzima.

Alisema zaidi ya mifugo 139,149 imezidi uwezo wa eneo la malisho hali inayosababisha uchungaji

katika maeneo yasiyoruhusiwa, ikiwemo misitu, maeneo ya kilimo na kusababisha migogoro na uharibifu wa mazingira.

Mkuu wa Wilaya, Mwanga alisema kero kubwa ni ya wafugaji kulisha mazao ya wakulima na kusababisha hasara wakati fidia ikiwa haiendani na thamani ya mazao husika.

"Chanzo cha migogoro hii ni viongozi ngazi za vijiji kushindwa kusimamia sheria na miongozo iliyopo pamoja na kupokea rushwa ili kuingiza mifugo kwenye vijiji," alisema Alhaj Mwanga.

Ahimiza wavuvi kushiriki sensa

Na John Gagarini,
Bagamoyo

NAIBU Waziri wa
Ardhi, Nyumba
na Maendeleo ya
Makazi, Ridhiwani Kik-
wete amewataka wananchi
kushiriki sensa ili waweze
kujiletea maendeleo.

Ridhiwani aliyasema hayo
wilayani Bagamoyo alipozung-
umza na wadau wa uvuvi
na mifugo na wananchi juu ya
umuhimu wa kushiriki kwenye
sensa.

Alisema kuwa sensa
ni maendeleo, hivyo ni
lazima kila mmoja ahakikishe
anashiriki ili aweze kuhes-
abiwa na serikali iweze kuleta
maendeleo kutokana na idadi
ya watu.

"Moja ya dodoso kubwa
ambalo wizara ya ardhi imeli-
toa ni kutambua nyumba na
makazi ya wananchi, hivyo ni
muhimu ili kutambua idadi ya
watu wanaoishi kwenye nyum-
ba na makazi yao," alisema
Ridhiwani.

Ridhiwani ambaye pia ni
Mbunge wa Chalinze alisema
sensa itasaidia kutambua idadi
ya watu na makazi yao, hivyo
kurahisisha upelekaji maende-
leo.

"Tutapata maelezo ya
kina juu ya kupanga maende-
leo yetu hivyo zoezi hili ni
muhimu sana kwa nchi yetu.
Hatuna budi kushiriki ili
tuweze kuletewa maendeleo,"
alisema Ridhiwani.

Aidha, alisema kuwa
idadi ya watu inapofahamika
inakuwa ni rahisi kujua mahi-
taji yao na kuwezesha serikali
na taasisi zake kupanga vizuri
bajeti ya maendeleo ili huduma
muhimu ziweze kupatikana.

"Nawasihi sana Wanabaga-
moyo, Wanapwani na Watan-
zania wote kushiriki zoezi hili
itakapofika Agosti 23, mwaka
huu kwani sensa ni muhimu
na pia maendeleo," alisema
Ridhiwani.

UHURU UK 9.

SH. 100,000>>Kiwango cha faini wanachotozwa wafugaji wan

* RC ataja sababu wafugaji kutengewa ekari 30,000 *

Na LATIFA GANZEL, Morogoro

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigella, amesema wametenga ekari 30,000 kwa wafugaji ikiwa ni miongoni mwa hatua za kudhibiti migogoro baina ya wafugaji na wakulima.

Shigella aliyasema hayo mkoani hapa juzi wakati wa mkutano na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki na wadau wa mifugo uliofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

"Eneo hilo wafugaji watatakiwa kupanda nyasi za malisho kuokoa mifugo yao, nyakati za ukame," alisema.

Shigella alimuomba Waziri Ndaki

kuitisha kamati ya wanasheria kutafsiri upya sheria ya faini ya mifugo, pale inapobainika wafugaji wamezivunja kwa kuwa zilizopo zinakakasi katika kuzitekeleza.

«Zipo zinazotaja faini ya shilingi 100,000 kwa tukio na ile inayotaka kuhesabu idadi ya mifugo na kila mfugo kulipiwa shilingi 100,000,» alibainisha.

Kuhusu mipaka iliyowekwa kati ya mwaka 2012, 2015 na 2017 katika bonde oevu la Kilombero, kulitenganisha na shughuli za kibinadamu, Shigella alieleza uamuzi wa sasa ni kufuata mpaka wa mwaka 2017 ulioelekezwa kupitia kamati ya mawaziri wanane.

Alisisitiza lengo ni kuondoa migongano ya kutofahamu iwapo

mifugo ipo nje au ndani ya hifadhi au shughuli za kilimo zinafanyika eneo sahihi ama la.

Waziri Ndaki aliwataka wakuu wa mikoa kufanya mikutano baina ya wafugaji na wadau wengine wa ufugaji, kutatua changamoto kwa pamoja.

Alisisitiza umuhimu wa pande zote kuheshimu misingi ya kisheria iliyowekwa kuleta uwajibikaji na kuondoa malalamiko ya wafugaji.

«Sasa tusaidiane kuwabaini hao wasio waaminifu na waliokuwa kero kwa wafugaji, tuchukue hatua stahiki. Lakini na wafugaji muache mara moja tabia ya kupeleka mifugo hifadhini,» alisema.

Mbunge wa Jimbo la Mikumi (CCM), Dennis Londo, akizungumza kwa niaba ya wabunge wa mkoani hapa, aliomba serikali iruhusu mifugo kuingia maeneo ya mapori ya akiba kwa kuwa inakula majani pekee.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji, Kata ya Parakuyo, Kalaika Motosyo, aliomba serikali kutoa elimu zaidi kwa wafugaji kuhusu uvalishaji mifugo hereni za kielektroniki kwa utambuzi.

THE GUARDIAN Page 5.

* NARCO embarking on nationwide crackdown to curb encroachment *

By Correspondent Valentine Ofora, Dodoma

THE National Ranching Company Limited (NARCO) has embarked on a special crackdown to control a spate of illegal human infringement at its ranches across the country.

There have been reports on illegal human activities within the NARCO earmarked ranches, the thing that ~~thwarts~~ performance of the state-owned company towards attaining its set targets in upgrading performance of the vital economic sector.

Prof Peter Msoffe, NARCO Director General told The Guardian that invasions into earmarked ranches stands a great barrier which retards efforts to improve NARCO's standards, pace of service delivery as well as animal's welfare and security.

He said the company had already re-surveyed earmarked and placed permanent boundaries to all of its ranch blocks to ensure sustainability of security services and animal's welfare.

The ranches that are prone to the said encroachment includes the Mkata ranch in Morogoro Region as well as those in Kagera Regional, namely Mabale, Kikulula, Misenyi, Kitengule, Kagome and Mwisu II.

"Apart from placing permanent boundaries, we are running a special campaign to raise awareness among communities dwelling adjacent to the ranches over the need to discourage dishonest tendencies of intruding into ranches areas, and instead, to maintain mutual relationship with our staff at ranches," he insisted.

He said the company also plans to employ at least 64 new staff who will be deployed to handle diverse departments.

"The company used to experience a challenge of shortage of human resources, we thank the government for allowing us to recruit new staff to fill the existing gaps," he said.

The company is currently undergoing major reshuffle with an eye to enable it to operate as a full business oriented entity, being undertaken by the newly introduced board of directors under the chairmanship Eng. Cyprian Luhemeja.

With a general vision to improve its service delivery and income, NARCO now envisioned to procure standard breeding stock from within and outside the country as part to improve livestock breeds among the pastoralists in the country.

The other envisaged economic project includes procurement of key facilities for expansion of grazing areas within the two major ranches of Kongwa and Mzeri in Dodoma and Tanga respectively.

In Tanzania, the livestock industry plays important socio-economic roles that include contributing to building a strong national economy, contributing to household food supplies and incomes and in providing employment opportunities to livestock keeping individuals and communities, while nurturing the natural resources.

The country has a total area of 945,000km² whereas 62,000km² of the surface area is covered water and has 60 million hectares of rangelands that are suitable for livestock production.

The available rangeland resources and varied forage and fodder resources are suitable for grazing to the available 28.4 million cattle; 16.7 million goats and 5.01 million sheep, 1.85 million pigs, 37.4 million indigenous poultry and other non-conventional species such as donkeys and rabbits.

The National Ranching Company Limited (NARCO) is a parastatal organisation under the Ministry of Livestock and Fisheries responsible for large scale commercial j ranching in the country.

The company is currently undergoing rapid transformation intended to create an efficient and vibrant commercial entity that will contribute very positively to the commercial development of the country's livestock industry.

"The company used to experience a challenge of shortage of human resources, we thank the government for allowing us to recruit new staff to fill the existing gaps"



RUWASA kukamilisha mradi bwawa kunyweshea mifugo

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAKALA wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), unatarajia kukamilisha mradi wa maji na bwawa kwa ajili ya kunyweshea mifugo kwenye Kijiji cha Msomera wilayani Handeni mwishoni mwa mwezi Julai, mwaka huu.

Kijiji hicho kilikumbwa na uhitaji wa maji baada ya wa-

nanchi kutoka Ngorongoro waliohamia eneo hilo kwa hiari. Mkurugenzi Mkuu wa RUWASA, Clement Kivegalo, akizungumza juzi na waandishi wa habari, alisema RUWASA inatekeleza ujenzi wa mradi wa maji katika kijiji hicho na mpango wa utekelezaji uligawanywa katika awamu mbili.

Alisema awamu ya muda mfupi imekamili na vituo vya kuchotea maji 12 vime-

shaanza kutoa huduma ya maji.

"Awamu ya pili imefikia asilimia 70 na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Julai, 2022. Kukamilika kwa awamu hiyo kutawezesha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wapatao 17,000 pamoja na mifugo yao na kufanya idadi ya vituo vya maji kuongezeka kutoka 12 hadi kufikia vituo vya kuchotea maji 30 kwa matumizi ya binadamu

na vituo tatu vya kunyweshea maji mifugo," alisema.

Aidha, alisema kuboresha huduma ya maji katika Kijiji cha Msomera, serikali kupitia RUWASA inaendelea na ujenzi wa bwawa la maji kwa gharama ya Sh. bilioni 1.99 na kwa sasa umefikia asilimia 15.

"Ujenzi wa bwawa hili utakapokamilika, utasaidia kuboresha huduma ya maji kwa wananchi na mifugo yao pia," alisema.